

**HOTUBA YA MHE. JOHN V.K. MONGELLA, MKUU WA MKOA  
WA MWANZA WAKATI WA KUADHIMISHA MIAKA 50 YA  
KITUO CHA UTAMADUNI CHA BUJORA NA SHEREHE ZA  
MAVUNO (BULABO) TAREHE 18 JUNI, 2017**

Mhe. Mwl. Hadijah Rashid Nyembo, Mkuu wa Wilaya Magu,

Mhashamu Thaddaeus S. Ruwa'chi, Askofu Mkuu, Jimbo Kuu  
Katoliki Mwanza,

Padri Fabian Muhoja, Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni  
Bujora,

Mhe. Mark Bomani, Mshauri wa Kituo cha Utamaduni Bujora,

Mhandisi Leonard Kadashi, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi  
ya Jubilei hii,

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya,

Waheshimiwa Mapadre, Watawa,

Wahe. Viongozi wa dini,

Ndugu Wanafamilia,

Wageni wote,

Mabibi na Mabwana,

Waandishi wa Habari,

Itifaki imezingatiwa.

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi  
Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutulinda na kutuwezesha

kukutana hapa leo. Vilevile kwa niaba ya wakazi wa Mkoa wa Mwanza, napenda nianze kwa kuwashukuru sana nyote kwa kutenga muda wenu ili tushirikiane kwa pamoja katika kuzindua Jubilei hii ya miaka hamsini ya kituo cha utamaduni na makumbusho ya Wasukuma Bujora, mmenionesha upendo mkuu na kunithamini kwa uamuzi wenu wa kunialika kuwa mgeni rasmi. Asanteni sana

Pili, naomba niwapongeze wamissionari kwa kazi nzuri walizofanya katika juhudi za kukusanya na kutunza urithi wa utamaduni wetu. Ninawapongeza pia uongozi wa kanisa katoliki, (Mhashamu Baba Askofu Mkuu) na uongozi wa kituo cha utamaduni Bujora, kwa kuthamini na kuendeleza kazi hii njema, mmeonesha mfano mzuri sana na wa kuigwa na kila mmoja wetu. Endeleeni na moyo huo, kama sehemu ya wajibu wa kila mmoja katika kuleta maendeleo kwa watanzania. Mimi mwenyewe nimejionea kazi hii njema, na juhudi mbalimbali za makusudi katika kutunza na kuendeleza tunu bora za utamaduni wetu. Hongereni sana na wote kwa pamoja tuendeleo kusonga mbele bila kukata tamaa.

**Ndugu zangu,** Utamaduni ni maisha kwa ujumla wake, ni kitambulisho cha kila mtu na kila Taifa. Taifa lisilo na utamaduni ni kama taifa lilokufa. Sisi watanzania tumerithi utamaduni mzuri sana toka kwa mababu zetu, lakini kwa sababu ya changamoto ya utandawazi na mwingiliano wa mila na desturi za kigeni, ipo hatari ya kupoteza utamaduni wetu, kwa

sababu hiyo, Serikali inaunga mkono yeyote mwenye nia njema, anayefanya juhudi za kuenzi tunu bora za utamaduni wetu.

**Ndugu zangu,** Nichukue fursa hii kuwakumbusha watanzania wote kuenzi na kudumisha utamaduni wetu, ingawa si vibaya kuiga utamaduni wa kigeni ulio mzuri, lakini pia ni vibaya kuacha utamaduni wetu ulio mzuri. Naomba nitoe wito wa kila mmoja wetu kuuthamini, kuutunza, kuuonesha na kuenzi urithi wa utamaduni wetu.

**Ndugu zangu,** Katika risala ya Mkurugenzi wa Kituo, amezungumza kuwa, tamasha hili la ngoma na nyimbo ni kusherekea Mavuno ya chakula baada ya kazi ngumu za kilimo. Nichukue fursa hii kuwapongeza wote waliofanya kazi za kilimo kwa bidii na kupata chakula cha kutosha. Kufanya kazi kwa bidii kumbe ni utamaduni wetu, uzembe na kutofanyakazi sio utamaduni wetu. kila mmoja wetu na afanye kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo na baada ya kazi tunapata nafasi ya kupumzika kwa michezo ya ngoma, nyimbo na burudani mbalimbali.

**Ndugu zangu,** Kufanyakazi kwa bidii kunaendana na kutunza chakula na kukitumia vizuri kwa faida ya familia nzima. Naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza waliobahatika kupata chakula cha kutosha, tusikitumie vibaya chakula tulichopata bali tukitumie vema na tukumbuke

kuweka akiba kwa wakati ujao ili kuepuka upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza.

**Ndugu zangu,** Nimefurahishwa sana na jinsi mlivyoona umuhimu wa kuendesha Tamasha hili mkiunganisha na kauli mbiu ambayo kila mwaka inajadiliwa na kukubaliwa na wadau wote kwa lengo la kuelimisha jamii, mmefanya ubunifu mzuri sana wa kufikisha ujumbe muhimu kwa watu kwani ujumbe unazungumzwa kwa Lugha ya nyumbani na hivyo kufika kwa urahisi zaidi na kwa njia ambayo inaeleweka takribani kwa wote.

**Ndugu zangu,** Ninapenda kuungana nanyi kwa kauli mbiu ya mwaka huu ambayo inasema **“Utamaduni na Kazi”** kuwaalika kila mmoja wetu kupenda, kuthamini na kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo yetu sisi na ya Taifa kwa ujumla.

Tukumbuke kwamba, Mwenyezi Mungu amependa na ametupatia Nchi hii ya Tanzania kuwa yetu sote, hatuna sehemu nyingine ya kujivunia na kuishi kwa Amani na Upendo zaidi ya Tanzania. Mshikamano na umoja wa kitaifa ni tunu bora tuliyorithi na ambayo ni wajibu wa kila mmoja kuhakikisha kuwa unaendelea na kurithisha kizazi kijacho. Amani ni utamaduni wa watanzania, hatuna budi kuienzi siku zote.

**Ndugu zangu,** Ninawapongeza sana kamati ya maandalizi ya jubilei hii, Chini ya Mwenyekiti wake Mhandisi Leonard Kadashi, kwa juhudi mlizofanya kuhakikisha kuwa Mnafanikisha kazi hii njema, tunawaalika pia watu wote wenye mapenzi mema

kujitokeza na kufadhili maadhimisho haya, kadiri ya Programu tuliyosikia. kwa kufanya hivi tutakuwa tunaendeleza upendo na udugu kati yetu na kuonesha kujali utamaduni wetu.

**Ndugu zangu,** Ninawahakikishia kuwa Serikali inathamini sana utamaduni wa Mtanzania na ninawaahidi kuwa Serikali itaendelea kutoa mchango wake kadiri nafasi inavyoruhusu na kwa wakati ili utamaduni wetu udumu siku zote.

**Ndugu zangu,** Mwisho, tunapozindua leo Jubilei hii ya Dhahabu, nimalizie kwa kuwashukuru tena kwa kazi njema za maandalizi mazuri, niwahakikishie kuwa niko pamoja nanyi katika juhudi zenu zote. Nawatakieni kila jema katika kudumisha utamaduni wetu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza